# MWISHO WA MUHULA WA KWANZA - 2020
# DARASA LA SITA - KISWAHILI: LUGHA

***Muda: Saa 1 Dak. 40***

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 - 15. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Waziri wa___1___Bw. Mawe ameagiza___2___ardhi___3___itakayotengewa___4___na serikali,lazima iandamane na stakabadhi rasmi. B.w. Mawe alisema___5___zitamsaidia kutetea wizara yake bungeni na mbele ya___6___. "___7___rais na kamishna wa ardhi___8___mamlaka ya kugawa ardhi ya umma,___9___muhimu ikiwa___10___kama___11___utafanywa chini ___12___katiba." Bw. Mawe alisema. Bw. Mawe___13___maafisa katika wizara hiyo kuwa na ___14___ na uwajibikaji katika kutenda kazi___15___. "Jambo hili lingekuwa na manufaa kwa wananchi wote." Bw Mawe akaongeza.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. Adhi | B. ardhi | C. Ardhi | D. ardhini |
| 2. | A. kuwa | B. kua | C. ka | D. kukuwa |
| 3. | A. lote | B. yote | C. zote | D. kote |
| 4. | A. yeyote | B. yoyote | C. wowote | D. wote |
| 5. | A. stakabadhi hio | B. stakabathi zake | C. stakabathi hiyo | D. stakabadhi hizo |
| 6. | A. umati | B. umma | C. uma | D. kadamnasi |
| 7. | A. Yapo | B. Iwapo | C. Endapo | D. Ingawa |
| 8. | A. ana | B. wako | C. ako | D. wana |
| 9. | A. itakuwa | B. itakuaa | C. Itakuwa | D. atakuwa |
| 10. | A. ugawajii | B. ugari | C. ugomvi | D. ugawaji |
| 11. | A. hiyo | B. hio | C. huyo | D. huo |
| 12. | A. na | B. wa | C. ya | D. za |
| 13. | A. aliwaita | B. aliwataka | C. aliwakashifu | D. kashifu aliwagombeza |
| 14. | A. wasiwasi | B. wazi | C. wasi | D. uwazi |
| 15. | A. yao | B. zao | C. wao | D. kwao |


***Kuanzia nambari 16 ahdi 30 jibu kulingana na maagizo***

16. Sina uzi_____mfukoni.
A. wowote B. yoyote
C. zozote D. popote

17. Majira ya mvua kubwa hujulikana kama____
A. dhoruba B. tafani
C. kusi D. masika

18. Andika sentensi hii kwa udogo:
**Mbwa yule anabweka**
A. kimbwa kile anabweka
B. kijibwa yule anabweka
C. kijibwa kile kinabweka
D. jibwa lile linabweka

19. Sehemu hii ya ndege inajulikana kama




A. kidona B. mdomo
C. kucha D. kudona

***Tumia nomino kundi ipasavyo***

20. Bibi ametuzwa kwa kupatiwa leso nyingi
A. doti la leso B. jozi ya leso
C. bumba la leso D. bunda la leso

21. Nimepitisha umri wa miaka mia moja.
A. kame B. mwongo
C. darzeni D. korija

22. Kamilisha tashbihi, ghafla kama_____
A. ajali B. umeme
C. upote D. upinde

23. Panda ni kwenda juu ya kitu au kuweka mbegu au miche ardhini ili imee au ikue, vile vile panda ni______
A. ala B. manati
C. samaki D. aina ya chombo

24. Ufipisho wa:
**Shemeji yake ni_______**
A. shemejiku B. shemejiye
C. shemejie D. shemeji yake

25. Mkoba wake ni_______
A. mieusi B. nyeusi
C. mweusi D. jeusi

26. Jina ua ambalo lina maana ya mzunguko wa boma liko katika ngeli ya________
A. LI - YA B. U - I
C. U - ZI D. U - U

27. Mama alitandika_______
A. kochi B. meza
C. zulia D. rafu

28. Yai ______ni_____
A. lema/hili B. njema/hii
C. jema/hili D. njema/hili

29. Mlio mkali wa kufahamisha hali ya hatari kama vile gari la wagonjwa au la polisi huitwa________
A. king'ora B. kamsa
C. kuwika D. kubweka

30. Unataka nyumba yake ijengwe______?
A. upi B. yupi
C. ipi D. vipi

***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Kutokana na uchunguzi wa hivi majuzi, hali ya anga imebadilika kwa kuwa na joto jingi zaidi ya kiwango cha kawaida. Hili ni jambo ambalo limewafanya wanasayansi kutoka ulimwengu kote kuungana pamoja na kuanza kutafuta suluhu la janga hili. Joto jingi mara nyingi huleta maafa ya watu na wanyama.

Mojawapo ya sababu za hali hii ni moshi wenye gesi za kemikali hatari kutoka viwandani. Moshi huu huweza kuyeyusha ozoni ambayo ni mwavuli wa miale yenye nyuzi za juu zaidi kufika ardhini. Inapoyeyushwa, miale hii hufika ardhini moja kwa moja pasipo pingamizi lolote. Hali hii huleta joto jingi sana duniani.

La pili ni suala nyeti ambalo limekita mizizi hasa katika bara la Afrika. Nalo si lingine bali ni ukataji miti ovyo ovyo. Jambo hili limesababisha kuenea na kukua kwa jangwa. Ardhi iliyokuwa na

rotuba huchimbika na kuwa kavu na yenye mabonde yasiyolimika. Hatimaye matokeo huwa ni ukosefu wa chakula na lishe bora.

Suluhisho kuu la mambo haya mawili makuu ni kuwahamasisha watu wote kuhusu kuyatunza mazingira na uwajibikaji katika kuboresha mandhari yetu. Mandhari mema hatuzuia sisi kupatwa na maradhi na maisha yetu sote huboreka

31. Miti mingi ikiwa pamoja huitwa______
A. bahari
B. mlima
C. msitu
D. bustani

32. Mazao mengi hupatikana udongo ukiwa na
A. maji
B. rangi nyeusi
C. hewa
D. rotuba

33. Ukataji wa miti unaweza kusababisha
A. kuyeyuka kwa ozoni
B. kuenea kwa jangwa
C. mafuriko
D. baridi kali

34. Ni nini suluhisho ya hali ya anga?
A. Kupanda miti kwa wingi
B. Kuacha kutengeneza vitu viwandani
C. Kuwajibika katika kutunza mazingira
D. Kuziba mabonde

35. Taja mambo mawili ambayo yamesababisha hali ya anga kubadilika
A. mvua na baridi nyingi
B. kukata miti ovyo ovyo na gesi kutoka viwandani
C. kuchimbwa kwa rotuba ardhini
D. kutotunzwa kwa mazingira

36. Gesi zenye kemikali hatari hutoka wapi?
A. Ardhini
B. Barani Afrika
C. Viwandani
D. Kwenye jua

37. Wanasayansi wameungana kutoka
A. bara la Afrika
B. dunia nzima
C. bara uropa
D. jangwani

38. Wakati mrefu wa joto kali bila mvua huitwa msimu wa_______
A. kiangazi
B. vuli
C. masika
D. kipupwe

39. Uchunguzi kuhusu hali ya anga hufanywa na
A. wanahewa
B. wanasayansi
C. wanenaji
D. marubani

40. Kichwa kinachofaa kwenye hadithi hii ni
A. Athari za kuharibu mazingira
B. Umuhimu wa kupanda miti
C. Utabiri wa hali ya anga
D. Kuenea kwa jangwa

***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Mji huo ukiutazama kwa mbali unaweza ukadhani ni kurunzi za melikebu iliyotia nanga kilindini. Katikati kuna mnara wa kumbukumbu za wazalendo waliopigania uhuru wa taifa la Garsen. Ndani ya mnara ule kuna rafu zilizotundikwa baadhi ya vifaa walivyokuwa wakitumia wazalendo hao. Kuna chumba kimoja kitumikacho kama makavazi. Ndani kuta zake ni za dhahabu inayodhihirisha dhahiri kwamba tamaduni za nchi hiyo zimehifadhiwa katika hali ya juu sana.

Barabara zinazopita katikati mwa mji huo zimegawanywa mara mbili, kila upande ukiwa na magari kushoto na kulia. Vile vile nyua zake hazivukiki kwani miba ya maua ya waridi imepitana na kujitega

tayari kuwafunza adabu watovu wa nidhamu. Usiku kucha biashara hunoga sawa na mchwa kwani mitaa yote imewekwa majitaa makubwa yanayoangaza ja mbalamwezi. Huu ni mji wenye biashara chungu nzima.

Kando ya mji huo kuna safu ya milima iletayo mfano wa Yerusalemu ya enzi za masihi karne nyingi zilizopita. Juu ya vilima hivi kuna misitu inayohifadhi wanyamapori. Si ajabu kumsikia fisi akipiga kamsa zake alfajiri kuu. Chini ni mabustani ya mitunda iliyotunzwa vyema kabisa na makaburi ya waliosalia baada ya Garsen kujinyakulia uhuru.

Kutoka vilimani vile umeshuka Mto Tiva ukajipindapinda na kufanya mji huo kuonekana kama kisiwa. Upepo mwanana utokanao na anguko la maji la Mto Tiva linafanya mji ule kuwa na baridi shadidi. Ndio maana mji ule unaheshimika kwa kuwa na kiwango kikubwa cha watalii Barani Afrika. Hakika mji huu ni maarufu kwa mandhari yake na historia yake ya kuvutia.

41. Biashara katika mji unaozungumzwa
A. hufanywa asubuhi kunapokucha
B. huisha jioni
C. huendelea kwa saa ishirini na nne
D. hufanywa tu wakati wa usiku

42. Mtu anayependa nchi yake na yuko tayari kuifia huitwa
A. Rais
B. Mwananchi
C. Msaliti
D. Mzalendo

43. Wakati baada ya alfajiri kuu ni______
A. mafungulia ng'ombe
B. alfajiri changa
C. adhuhuri
D. usiku mkuu

44. Neno **nyakulia** limepigwa mstari, kinyume chake ni________
A. kabidhiwa
B. rushiwa
C. nyang'anywa
D. tuzwa

45. Kamsa anazopiga fisi ni______
A. mgurumo
B. maabara
C. mlio
D. kicheko

46. Misitu inayohifadhi wanyama pori kwa jina moja huitwa
A. makavazi
B. maabara
C. mbuga
D. pango

47. **Makaburu** ni wale
A. wananchi wazalendo
B. watu waliotawala wengine kwa mabavu
C. wakulima shupavu
D. wafanyikazi shambani

48. Fafanua maneno ***safu ya mlima***
A. milima mingi ikifuatana laini moja
B. milima mifupi
C. milima mirefu
D. milima iliyotapakaa

49. Ni mandhari yapi yanayovutia watalii kuja katika mji huu wa Garseni?
A. Nyua zake
B. Barabara zake
C. Anguko la maji Mtoni Tiva
D. Safu ya milima

50. Nchi inayozungumziwa inaitwaje?
A. Tiva.
B. Kafira
C. Garsen
D. Kenya